TAARIFA YA HATUA ZA MAANDALIZI YA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE KWA AWAMU

JANUARI, 2026

UTANGULIZI

Sheria: Bunge lilitunga Sheria hii ya Bima ya Afya kwa wote mwaka 2023

Sheria imeanza kutumika

TS Na. 700A

16 Agosti 2024

Kanuni za utekelezaji zimetangazwa

TS Na 809

13 Septemba 2024

2. DHANA YA BIMA YA AFYA

Bima ya Afya kwa Wote

Malipo kabla ya huduma

Utaratibu wa kulipia huduma za afya kabla ya kuugua. kwa kuwa na kiwango cha kuchangia

Uwajibikaji wa pamoja

- Serikali,
- Skimu za bima ya afya,
- Vituo vya kutolea huduma za afya,
- Wananchi.

Uchangiaji wa Pamoja

Kuchangia fedha katika kapu moja kwa ajili ya kupata huduma za afya (Mf. vikoba)

Huduma za afya

Upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wakati

Kuchangiana

Kati ya wenye uwezo na wasio na uwezo; wagonjwa na wasio wagonjwa

Usawa

Uchangiaji kwa kuzingatia uwezo na utoaji wa huduma za afya kwa kuzingatia mahitaji

3. MASUALA MAHSUSI KATIKA SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE



“Ndani ya siku 100 za utawala wangu, Tutaanza utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote kwa majaribio kwa baadhi ya **makundi maalumu yasiyokuwa na uwezo** yakiwemo ya **wazee, watoto, wajawazito na watu wenye ulemavu**” Ahadi ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mgombea wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) wakati wa uzinduzi wa Kampeni.

4. UTEKELEZAJI WA BIMA YA AFYA KWA WOTE

- Usajili wa wananchi katika Bima ya Afya utatekelezwa kwa awamu kwa baadhi ya **makundi maalumu yasiyokuwa na uwezo yakiwemo ya** wazee, watoto, wanawake wajawazito na watu wenye ulemavu ambao watagharamiwa na Serikali.

A. Kuandaa na kukamilisha miongozo mbalimbali

a. Mwongozo wa **uendeshaji na usimamizi wa mfuko wa kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo**;

b. Mwongozo wa **usajili wa skimu za bima ya afya**;

c. Mwongozo wa **Utambuzi wa watu wasio na uwezo**;

d. Mwongozo **usajili wa wanachama**;

e. Mwongozo **ulipaji wa madai**;

f. mwongozo wa **rufaa wa upatikanaji wa huduma za afya**.

B. Kuboresha mifumo ya TEHAMA



C. Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya

Kujenga uwezo wa wataalam.

Kuongeza idadi ya watumishi.

Kujenga vituo vya kutolea huduma za afya

Kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa

Kuimarisha mifumo ya tiba mtando (telemedicine).

Kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tima

Bodi za udhibiti ubora wa huduma za afya

D. Kukamilika kwa kitita cha mafao chenye huduma 372 kwa gharama ya TZS 150,000

Vigezo vya uandaaji wa kitita cha mafao ya Bima ya Afya kwa wote;

Malengo ya kisera

Kama vile kupunguza vifo vya mama na mtoto;

Uwiano (Equity)

Usawa katika upatikanaji wa huduma za afya ikijumuisha makundi maalum ikiwa ni pamoja na wajawazito, watoto chini ya miaka mitano na wazee

Mzigo wa magonjwa (burden of disease)

Ujumuishaji wa huduma zinazohusiana na magonjwa yanayoathiri asilimia kubwa ya wananchi;

Uhatari wa ugonjwa (Severity of disease)

Ujumuishaji wa huduma za magonjwa ambayo yanachangia kusababisha vifo na madhara makubwa ya Kiafya kwa haraka (Morbidity and Mortality).

Ustahimilivu / Ulinzi wa kifedha wa Mfuko:

Utoaji wa baadhi ya huduma umeangalia uwezo wa kuhimili gharama ili kulinda uhai wa mfuko

Huduma za Uchunguzi

Huduma za vipimo vya

- Maabara- **43**
- Radiolojia **-37**

- Huduma hizi zimejumuisha huduma za vipimo vyote vya ngazi ya msingi
- Imejumuisha huduma 3 zinazotolewa ngazi ya rufaa (ABG, Glucose Tolerance Test)

Huduma ya Dawa na Vifaa Tiba

Huduma ya dawa na vitendanishi **247**

- Imejumuisha dawa za ngazi A,B, C hadi D
- Kitita kina dawa 2 ambazo zipo katika ngazi S (Hydroxyurea na Insulin Injection)
- Kitita kimejumuisha dawa zote za ngazi A-D kwa kuzingatia nguvu na muundo wa dawa zote hivyo kuongeza wigo wa huduma ya dawa ukilinganisha na idadi ya dawa zilizoainishwa

Huduma za Upasuaji

Huduma **37** za upasuaji mkubwa na mdogo

- Huduma za msingi za upasuaji na baadhi ya huduma za upasuaji mkubwa zinazotolewa katika ngazi ya rufaa
- Huduma zimechaguliwa kwa kuzingatia vigezo vya usawa, uhitaji na uokoaji wa maisha.
- Kipaumbele kimetolewa kwa huduma zinazochangia kupunguza vifo vya mama na mtoto na ajali.

E. Utambuzi wa watu wasio na uwezo

- Katika utambuzi wa watu wasio na uwezo;
  - Jumla ya wananchi **3,695,465** sawa na kaya **931,693** **wa**metambuliwa, (ikiwajumuisha wanawake wajawazito na watu wenye ulemavu wasio na uwezo)
  - **Wazee 229** na **watoto 267** wanaohudumiwa na katika vituo maalaum chini ya Wizara MJJWMM wametambuliwa
  - Katika awamu ya kwanza jumla ya wananchi **1,457,602** sawa **kaya 276,004**; **Wazee 229** na **watoto 267 watasajiliwa na kugharamiwa na Serikali.** **(wananchi hao wanapatikana katika Halmashauri zote Nchini)**
- Wigo wa utambuzi utaendelea kuongezwa ili kuwafikia wananchi **16,845,065** **sawa na kaya 3,917,457 (Takwimu za NBS)**

F. Commitment ya Serikali ya Awamu ya Sita

TZS Bilioni 587.6

- Mahitaji Halisi ya Kaya zisizokuwa na uwezo

TZS Bilioni 201

- Bajeti ya mwaka 2025/26

TZS Bilioni 48.8

- Kiasi kilichotolewa

G. Utaratibu wa Rufaa



5. MAJUKUMU YA WASHIRIKI WA MKUTANO

- Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika mamlaka zao **kuhakikisha wanaweka mazingira mazuri ya utoaji elimu na uhamasishaji wananchi** kuhusu mpango wa bima ya afya kwa wote;

- Makatibu Tawala wa Mikoa na wilaya pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha **wanaratibu na utoaji wa elimu na uhamasishaji wananchi** kuhusu mpango wa bima ya afya kwa wote;

5. MAJUKUMU YA WASHIRIKI …

- Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuendelea **kusimamia upatikanaji wa huduma bora za afya** kwa wananchi katika maeneo yao;

- Kushirikiana na **mamlaka za utambuzi katika kutambua wananchi wasio na uwezo watakaogharamiwa** na Serikali Bima ya Afya kwa Wote;

- Agenda ya Bima ya Afya kwa wote **iwe agenda ya kudumu katika vikao vya RCC na DCC** (Taarifa ya utekelezaji wa malengo yaliyowekwa katika mkoa na Wilaya husika kujadiliwa); na

5. MAJUKUMU YA WASHIRIKI …

- Makatibu Tawala wa Mikoa na Halmashauri, pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri, kuhakikisha Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri, na Waganga Wafawidhi wa Vituo vya kutolea huduma za afya **wanasimamia ubora wa huduma za afya katika vituo vyao ili iwe chachu ya kuwavutia wananchi** kujiunga na mpango wa bima ya afya kwa wote.

Four million parts, 30 countries: How an Airbus A380 comes together

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA

USIMAMIZI NA UDHIBITI WA MFUMO WA BIMA YA AFYA KWA WOTE

JANUARI, 2026

6. MAJUKUMU YA TIRA

Pamoja na majukumu mengine, Mamlaka ina majukumu mahususi yafuatayo:-

i. **Kusajili na kutoa leseni** kwa watoa huduma za bima (insurance registrants);
ii. **Kusimamia sekta ndogo ya bima nchini ikiwemo kutoa Miongozo ya usimamizi** wa Sheria na kiutendaji kwa watoa huduma za bima;
iii. **Kulinda maslahi ya walaji na wanufaika** wa huduma za bima;
iv. **Kuendeleza sekta ndogo ya bima** nchini; na.
v. **Kuishauri Serikali kuhusu sera na masuala mengine** ya bima nchini.

6. MAJUKUMU YA TIRA…2

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima ya afya kwa wote, TIRA ina majukumu yafuatayo;

i. **Kusajili Skimu za Bima ya Afya** (ikiwemo Skimu ya Bima ya Afya ya Umma – NHIF na Skimu Binafsi);

ii. Kuhakikisha **skimu za Bima ya Afya** zinatoa **kitita cha mafao ya huduma muhimu** kwa mujibu wa Sheria;

iii. **Kuhakikisha huduma za Bima zinazotolewa** zinaendana na viwango vya michango;

iv. **Kutoa miongozo ya usajili na malipo** kwa watoa huduma;

6. MAJUKUMU YA TIRA…2

v. **Kuhakikisha Skimu za Bima ya Afya zina ukwasi na akiba** ya kutosha kwa mujibu wa Sheria;

vi. **Kutunza kanzidata ya vituo vya kutolea** huduma za Afya vilivyoingia mikataba na skimu za Bima ya Afya;

vii. **Kufanya kaguzi za skimu za Bima ya Afya** ili kuhakikisha kuwa zinatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria;

viii. Kutoa **elimu kwa Umma kuhusu umuhimu** wa Bima ya Afya; na

ix. **kufanya tafiti** kwa lengo la **kuendeleza ufanisi na uendelevu** wa mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote.

7. KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO NA MIGOGORO YA BIMA

A. Kupokea na Kushughulikia Malalamiko:

Katika kuhakikisha wateja na wanufaika wa Bima wanapata **huduma bora za bima** kwa mujibu wa **Sheria na Kanuni**. TIRA:

- Imeandaa **Miongozo ya kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusu madai** na **utoaji wa huduma za bima;**
- **I**meainisha utaratibu wa kupokea **Malalamiko** kutoka kwa wadau wa Bima kwa lengo la **kutatua changamoto** wakati wa utoaji wa **huduma za Bima za Afya**.

Hatua za kushughulikia Malalamiko



7. KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO NA MIGOGORO…..

B. KUPOKEA NA KUSHUGHULIKIA MIGOGORO:

- **Kifungu cha 34 cha Sheria ya Bima ya Afya** imeeleza kuwa utaratibu wa kushughulikia Migogoro utakuwa kama ulivyoainishwa katika Sheria ya Bima Sura 394;
- Usuluhishi wa Migogoro ya Bima hufanyika kupitia **Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima (Tanzania Insurance Ombusman);**
- Migogoro ya Bima inashughulikiwa kupitia taratibu zilizoainishwa katika Kanuni za usuluhishi wa Migogoro ya Bima **(GN 411 za mwaka 2013).**

7. KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO NA MIGOGORO……

Hatua za kushughulikia Migogoro ya Bima



8. HITIMISHO

Afya si gharama. Afya ni uwekezaji wa kimkakati katika utu wa Mtanzania, uzalishaji wa uchumi, usalama wa taifa, na heshima ya nchi yetu. Hakuna Taifa imara juu ya watu dhaifu kiafya.

*Kwa pamoja twendeni tukatekeleze Ahadi ya **Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa kwa wananchi ya kuwawezesha kupata **Bima ya Afya***

Naomba Kuwasilisha

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA

1. USAJILI WA WANACHAMA

i. Kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kufungua ofisi katika maeneo 10 ya kimkakati(Masasi,Tunduma, Tegeta, Kahama, Bukombe, Katoro, Karagwe, Ifakara, Mbinga na Nzega (Kutoka ofisi 32 hadi 42 Nchi nzima)

ii. Kuwezesha mwananchi kujisajili mwenyewe online **(Self service portal)**

iii. Kutumia mawakala wa bima ambao wapo Nchi nzima

iv. Kutumia makampuni ya simu

v. Kuingia makubaliano na Tume ya Ushirika (**TCDC)**

2. Malipo Ya Madai kwa vituo vya kutolea huduma

- Malipo ya madai ya kitita hiki yatakuwa kwa kutangulizwa kwa mkupuo (Capitation) na mfumo wa sasa wa *Fee for Services* kutegemeana na makubaliano na kituo

- Vituo vinavyomilikiwa na watoa huduma binafsi na madhehebu ya dini vitaruhusiwa kutoa huduma kwa kufuata misingi na taratibu zilizowekwa

3. Fursa ya Mikopo kwa Watoa Huduma

- Mpango wa Mikopo ya vifaa vya tiba, dawa na ukarabati inakusudia kutoa mikopo ya ununuzi wa vifaa tiba, dawa, ukarabati kwa vituo vya kutolea huduma vilivyosajiliwa. Aina ya vifaa ni vile vyote vilivyoidhinishwa kutumika katika vituo.

- Masharti ya mikopo ni nafuu kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa wakopaji. Baadhi ni:-
  i. Vituo hivyo vitapewa vifaa/ dawa na si fedha taslimu
  ii. Mkopaji atafuata taratibu za manunuzi zilizoidhinishwa chini ya Sheria ya Manunuzi
  iii. Mikopo inatolewa kwa vituo vya afya vilivyosajiliwa
  iv. Kuwepo kwa idhini ya mmiliki wa kituo au mali isiyohamishika

4. Mikopo ya vifaa vya TEHAMA

Ili kurahisisha uwepo wa mifumo itakayosaidia utoaji wa huduma wakati wa utekelezaji wa sheria ya UHI, fursa ya mikopo itawezesha pia kupatikanaji kwa vifaa vya TEHAMA. Vifaa hivyo vinaweza kuwa mfumo mzima au sehemu;

i. Kompyuta na vifaa vyake;

ii. Vifaa vya mifumo ya Utambuzi (biometric identification devices); na

iii. Mifumo ya Umeme (Power back-ups).

- **Naomba Kuwasilisha**